## Jinsi ya kushiriki

### SHIRIKI KATIKA TAFITI ZETU

Utafiti mkuu umeanza hivi karibuni. Unakaribishwa sana kushiriki na kuunngamkono utafiti wetu. Wasiliana nasi kwa taarifa zaidi!

### KUTANA NA WATAFITI

Hudhuria mkutano wa hadhara katika eneo la utafiti wa UPSIDES ambalo lipo karibu yako. Wasiliana nasi kwa maelezo.

## Wasiliana nasi

### TEMBELEA UKURASA WETU

JE UNGEPENDA KUJUA SISI NI KINA NANI NA TUNAFANYA NINI? TAZAMA TOVUTI YETU!
https://www.upsides.org

### MITANDAO YA KIJAMII

Pata taarifa za hadi leo kupitia Twitter:@UpsidesProject

Jiandikishe katika jarida letu kwa kuwasiliana na UPSIDES@uni-ulm.de


TAARIFA ZA MAWASILIANO:

Ifakara Health Institute

Mr. Donat Shamba

+255683105670
dshamba@ihi.or.tz


JARIDA LIFUATALO: #05-JUNI 2020

→Uwezeshaji na vizuizi katika utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji rika wa UPSIDES.
→Mahojiano na Dr. Galia Moran (Israel)
→Fikiria mbele: Maandalizi ya kutekeleza mpango endelevu wa uwezeshaji rika wa UPSIDES.

Tuma habari yako kwa UPSIDES@uni-ulm.de ili itokee katika jarida lifuatalo!

# UPSIDES

# Jarida

#04 Machi 2020

## #04-MADA

### MAHOJIANO NA DR. CANDELARIA MAHLKE

Kiongozi wa work package 3 anaripoti jinsi mpango wa UPSIDES ulivyotengenezwa

### UTEKELEZAJI WA UWEZESHAJI RIKA

Soma zaidi kuhusu utekelezaji wa shughuli za UPSIDES katika maeneo/sehemu mbalimbali. Ni mikakati gani ilifuatwa katika sehemu zote? Na ni vitu gani husika vitakuwepo katika sehemu husika?

### KUANZA KWA JARIBIO LA KUDHIBITI NASIBU

Ufanisi wa uwezeshaji rika wa UPSIDES utapimwaje katika maeneo/sehemu mbalimbali?


UPSIDES imepokea ufadhili kutoka European Union Horizon 2020 programu ya utafiti na uvumbuzi chini ya makubaliano no 779263. Barua hii ya taarifa inaonyesha mtazamo wa waandishi tu. Tume haihusiki na taarifa zilizopo.


www.upsides.org

## Mahojiano na Dr. Candelaria Mahlke

*Q: Ni hatua zipi mlizofata katika kuandaa vitendea kazi vya mafunzo?*


Muongozo wa mafunzo uliandaliwa kwa hatua. Tulikusanya taarifa kwa kufuatilia miradi juu ya mafunzo kwa rika na mingozo ya mafunzo iliyotumika katika maeneo yenye uzoefu wa uwezeshaji rika. Tulindaa muongozo wa kwanza ambao ulijadiliwa na vikundi vya wataalamu katika kila nchi na kufanyiwa mabadiliko kulingana na mrejesho tuliopata. Muongozo uliopatikana ulijaribiwa katika mafunzo kwa wakufunzi mkutano uliofanyika Tanzania uliojumuisha wakufunzi wa rika wenye uzoefu, wawezeshaji rika na watoa huduma wa afya ya akili kutoka katika kila eneo kwa ajili ya kupitia zaidi na hatimaye kufanyia mabadiliko baada ya mafunzo ya majaribio katika maeneo yote ikifuatiwa na mijadala ya vikundi.

*Q: Mlipata changamoto zipi?*

Changamoto ilikuwa katika kuanzisha mradi/program ambayo inaweza kutumika katika nchi za hali ya chini, kati na juu kiuchumi na hivyo kuwa rahisi kuendana na maadili ya sehemu husika na ambayo inaweza kufanya kazi bila kutegemea namna huduma za afya ya akili zinavyofanyakazi na rasilimali katika nchi husika. Tuliweka msisitizo katika uzoefu ambao ulionekana kuwa sawa ulimwenguni katika uwezeshaji rika na urejeshwaji wa afya/kupona,bila kujali eneo na tofauti za kiutamaduni kwa kuwa na mtu pamoja nawe katika nyakati za changamoto za kiakili, ambaye anaelewa ulikotoka na kuwa pamoja katika kukuwezesha kutizama mbele katika njia ya urejeshwaji wa afya binafsi.

*Q: Nini mtazamo wako kuhusu muongozo wa mafunzo wa mwisho?*

Muongozo wa mafunzo na kitabu cha mazoezi kinachoendana vimekwekwa katika namna iliyo rahisi kutumika na kuendana na mazingira husika ya kila sehemu. Ilitakiwa kujenga msingi kwaajili ya mtandao wa uwezeshaji rika  na kutoa matumaini na jamii inayowezesha katika kusaidia kuwawezesha wanaoathirika na kupambana na unyanyapaa. “Mti wa uzima” dhana iliyotumika katika mafunzo ya rika huko Uganda imekuwa kiini katika mafunzo ambayo imeshauriwa mara kwa mara katika kipindi chote na humsaidia mtu  kuunganisha na hadithi yake binafsi na kutengeneza mitazamo kulingana na uwezo na rasilimali binafsi.




## Utekelezaji wa uwezeshaji rika wa UPSIDES

*Majaribio*

Meneo sita yamemaliza majaribio na mafunzo mwaka jana. Mafunzo yalifanyika katika lugha husika Gujarati (India), Luganda (Uganda), Swahili (Tanzania), Kiebrania (Israeli) and Kijerumani (Ujerumani). Mafunzo yalipokelewa vizur katika kila eneo. Sasa tupo katika hatua ya kuanza majaribio ya ujuzi wa mafunzo.

“Mafunzo yalinipatia eneo la kujielezea na ilinisaidia kufikiria kuhusu safari yangu ya kupata nafuu,malengo ya baadae na kunisaidia kuboresha ujuzi wangu katika ustadi wa mawasiliano.” Muwezeshaji rika PU site

*Utayari wa taasisi*

Sehemu zote zinazotekeleza mradi zilifanya warsha za uso kwa uso na wafanyakazi. Lengo lilikuwa kutambulisha mradi na kuandaa sehemu ya kazi ya wawezeshaji rika. Majadiliano yalikuwa juu ya huduma zilizolenga urejeshwaji wa afya ya akili na uwezeshaji rika katika kazi. Kulikuwa na mambo yaliyoleta wasiwasi kama ukosefu wa maelezo ya wazi juu ya majukumu ya wawezeshaji rika, kazi kuwa ngumu zaidi sababu ya wawezeshaji rika na uzoefu mbaya wa uwezeshaji rika viliibuka wakati wa semina katika maeneo mbalimbali. Hizi hoja zilifanyiwa kazi katika kupangilia utekelezaji. Baadhi ya maeneo yalihitaji maelezo zaidi ili kuhakikisha utayari wa taasisi zaidi ya  warsha moja na mikutano ya utambulisho wa mradi.

## Kuanza kwa jaribio la kudhibiti nasibu

*Muundo wa utafiti*

Utafiti wa RCT unalenga kuangalia umuhimu wa uwezeshaji rika katika maeneo sita kwa watumia huduma na wawezeshaji rika. Utafiti unatumia muundo wa orodha ya kusubiri na mpangilio katika makundi ni wa bahati. Washiriki wote katika kundi la udhibiti watapatiwa matibabu kama kawaida, pamoja na huduma za kawaida na watapatiwa wawezeshaji rika baada ya mwaka mmoja. Washiriki watakaopangiwa katika kundi la afua/majaribio watapata uwezeshaji rika mara tu baada ya kujiunga.

Matokeo tunayotarajia ni ujumuishwaji wa kijamii, uwezeshaji, kupata nafuu, afya ya akili, utendaji kazi na ubora wa maisha. Matokeo haya yatapimwa katika kipindi cha miezi kumi na mbili.

Mnamo Januari 2020, maeneo yote yanayotekeleza huu mpango yalianza mchakato wa kuajiri watumiaji huduma. Tafadhali wasiliana nasi ikiwa utapenda kushiirki au unamjua mtu atakayependa kushiriki kwenye mradi huu.